



Makala ya Utafiti

UAINISHAJI WA FONIMU ZILIZODHIHIRISHA UKAKAMAAJI KWA WAJIFUNZAJI WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA PILI KATIKA VYUO VIKUU NCHINI BURUNDI

^{1,*}Révoat Ndayizeye and ²Dkt.Elither Kindole

¹Mwanafunzi wa uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam& mhadhiri msaidizi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Ualimu cha Burundi (ENS-BURUNDI)

²Mhadhiri wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Received 11th August 2025; Accepted 12th September 2025; Published online 30th October 2025

IKISIRI

Utafiti kuhusiana na suala la ukakamaaji kwa wajifunzaji wa lugha ya pili (kuanzia sasa Lg2) umeongezeka miaka ya hivi karibuni. Makala hii imeshughulikia suala la ukakamaaji wa kimatamshi kwa wajifunzaji wa Lg2 katika vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi. Utafiti ulifanyika Jijini Bujumbura, Chuo Kikuu cha Ualimu (kuanzia sasa CKU) pamoja na Chuo Kikuu cha Burundi (kuanzia sasa CKB); vyuo vikuu ambavyo vina idara za Kiswahili nchini humo. Utafiti huu uliongozwa na Nadhariatete Teuzi ya Ukakamaaji (kuanzia NATEU) iliyoasisiwa na Han (2009). Nadhariatete hii inaangazia kuwa katika kuhamisha kaida za Lg2 kuna vipengele mbalimbali vya Lg2 vinadhihirisha ukakamaaji kuliko vingine kutokana na tofauti kati ya Lg1 na Lg2. Dai kuu la Nadharia hii ni kuwa baadhi ya vipengele vya lugha fulani katika lugha husika vinakakamaa zaidi kuliko vingine. Makala hii ilikuwa na lengo la kuainisha fonimu tu zilizodhihirisha hali ya ukakamaaji kwa wajifunzaji Warundi. Makala hii ilitumia sampuli ya watoataarifa ishirini sawa na kumi kutoka kila Chuo Kikuu. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya masimulizi ya hadithi. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2 walikakamaa kwenye baadhi ya fonimu za lugha lengwa. Hata hivyo, sababu za ukakamaaji hazijabainishwa wazi ingawa imedhihirika kuwa uhamisho wa kaida za lugha ya kwanza (kuanzia sasa Lg1) katika kujifunza Lg2. Makala hii ilihitimisha kwa kupendekeza tafiti fuatizi zichunguze vipengele vingine vya isimu matumizi kuwa wajifunzaji wa Lg2 wanakumbwa na hali hii ya ukakamaaji au la.

Maneno muhimu: lugha ya kwanza, lugha ya pili, lugha lengwa, ujiipatiaji lugha, ukakamaaji.

UTANGULIZI

Katika Taaluma ya Isimu kuna tafiti kadhaa zilizofanyika kuhusiana na ujifunzaji wa Lg2 kwa mfano Zheng (2010) anaonesha kwamba wajifunzaji wa Lg2 ambao wanaanza wakiwa tayari wanayo Lg1 huwa wanakabiliwa na tatizo kubwa la kukakamaa. Ukakamaaji ni hali ya mjiifunzaji wa Lg2 kuipata na kuimudu licha ya kuwapa kwa motisha, ufundishaji bora, vifaa tosha vya kufundishia, muda wa kutosha wa kuchangamana na watumiaji wa Lg2 n.k. na sababu nyingine mbalimbali. Kwa mfano vipengele vya Lg1 vinaweza kuingilia hatua za ufundishaji wa Lg2 kwa kaida mbalimbali hasa za matamshi.

Aidha, watoataarifa hubainisha kuwa hata mazingira pamoja na jami inayomzunguka mjiifunzajilugha yanaweza kusababisha ufanisi au uhamisho wa umilisi wa lugha wanayojifunza. Katika Nadhariatete Teuzi ya Ukakamaaji, Han (2009) anaeleza vipengele vya ujiipatiaji lugha na ukakamaaji kwa kubainisha michakato yote miwili kuhusiana na suala zima la ukakamaaji na ujiipatiaji lugha. Nadhariatete hiyo inaonesha kuwa vipengele vyote viwili, ukakamaaji na ujiipatiaji wa lugha vinatokea kwa kuchochewa na hali kama: Motisha katika ujifunzaji na ufundishaji, ingizo tosha katika ujifunzaji wa Lg2 pamoja na mazingira ya mjiifunzajilugha. Vitu kama hivyo ndivyo vinasababisha ujiipatiaji lugha (Chen, 2009). Hata hivyo, mawazo ya mtalaamu Long (1997) yanadai kuwa hali ya ujiipatiaji L2, au lugha ngeni, inashindikana baada ya balehe. Isitoshe, taffi zilizofanyika zinaonesha kuwa licha ya kuwa na vitu vyote hivyo hapo awali, motisha, ingizo la kutosha na mazingira mazuri ya mjiifunzajilugha; wajifunzaji wa Lg2 ambao wamefikia balele au zaidi hawawezi kufikia kiwango cha umilisi wa mzawa wa Lg1.

Utafiti wetu ulilenga kuchunguza ukakamaaji wa kimatamshi kwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili ikiwa Lg2. Baadhi ya mambo yaliyoshughulikiwa ni pamoja na ubainishaji wa fonimu zilizodhihirisha ukakamaaji. Makala hii, kabla ya kuendelea, ilianza na fasili ya dhana mbalimbali ikiwamo Lg2 na dhana ya ukakamaaji katika ujifunzaji Lg2.

UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

Sehemu hii inaangazia fasili ya dhana mbalimbali.

Dhana ya Ukakamaaji

Dhana ya ukakamaaji ilipendekezwa kwa mara ya kwanza katika taaluma ya isimu matumizi na Selinker (1972:150) kuwa ni tukio la kiisimu ambapo huwapata wajifunzaji wa Lg2 wenye umri zaidi ya ule wa balehe¹. Aidha, kwa mujibu wa Zheng (2010: 326) ukakamaaji ni miongoni mwa vizingiti au vikwazo katika mchakato wa ujiipatiaji Lg2 au ya kigeni. Kutokana na hali hiyo, ni jambo la muhimu kwa walimu na wanafunzi kuzingatia hili. Pia, mbinu mwafaka na zinazofaa zaidi zinahitajika kutumiwa na walimu au wawezeshaji ili kuwasaidia kuondokana na hali hiyo.

Ukakamaajiau ukomo wa ujiipatiaji kama ilivyobainishwa na Selinker (1972: 150) ni tukio au jambo ambalo linawapata wajipatiaji Lg2 na au lugha ya kigeni. Ukakamaaji unafasiliwa kuwa ni hali inayowapata wajipatiaji Lg2 ambao hushindwa kufikia kiwango cha umilisi wa mzawa wa lugha. Kwa maelezo rahisi kabisa ukakamaaji ni hali ya kushindwa kumudu baadhi ya vipengele vya kiisimu vya Lg2 au ya

*Mwandishi Sambamba: Révoat Ndayizeye,

¹mwanafunzi wa uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam& mhadhiri msaidizi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Ualimu cha Burundi (ENS-BURUNDI).

¹Tukizungumzia balehe ina maana miaka zaidi ya kumi na mine kama anavyodai Mtaalamu Lenneberg (1967).

kigeni, licha ya kuwa na ingizo la kutosha, motisha na kupata fursa ya kuona matokeo.

Hata hivyo, Selinker (1996) amefasili dhana ya ukakamaaji kuwa ni mchakato ambao mjifunzaji lugha hufikia ukomo katika lugha darajia au lugha mpito na hivyo kusitisha uendeleaji wa lugha darajia au kufanya kuwa hali ya kudumu. Tofauti na Selinker (1972; 1996) Ellis (1985) kwa upande mwingine anaona kuwa ukakamaaji ni dosari au muundo/umbo sahihi la lugha darajia. Kulingana na fasili hii, Ellis(1985) anaona kuwa ukakamaaji una hatua mbili, kama mchakato ya ambapo kwake hiyo, sio ukakamaaji bali jitihada za ujifunzaji lugha na matokeo ya mchakato huo. Matokeo ya miundo au maumbo yakifanana na Lg2 au lugha ya kigeni hiyo ni dosari na ikiwa miundo au maumbo haya yataendelea kutofautiana na Lg2 au lugha ya kigeni basi hizo ni doasari. Hata hivyo, fasili ya Brown (1994) inatofautiana na zile zilizotolewa na Selinker na Ellis ambapo yeye anatazama ukakamaaji kama ni matokeo ya athari hisivu chanya au hasi pamoja na mrejesho tambuzi (Brown, 1994).

Lugha ya Pili

Stern (1983: 22) anafasili dhana ya Lg2 kuwa ni lugha ambayo mtu hujifunza mbali na lugha ya mama yake na ambayo anaitumia kimawasiliano ndani ya nchi yake au mazingira ya mtu yule. Hivyo, kutokana na fasili hii nchini Burundi; lugha ya Kiswahili ni lugha ya pili, kwani hujifunza na kuitumia lugha hii wakiwa tayari wana lugha yao ya Kirundi katika maeneo yao wanamoishi. Katika kushadidia wazo hili. Mtesigwa (2009) anaeleza kuwa kutokana na ufafanuzi huu, tunaweza kusema kuwa Kiswahili ni Lg2 kwa watu wengi wa Afrika Mashariki ambao wana lugha za makabila yao na ambazo ndizo lugha mama walizozijua kabla ya kujua Kiswahili. Hivyo, utafiti kuhusu athari za lugha mama katika ujipatiaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama Lg2 haujafanyika vya kutosha. Kuna haja ya kufanya utafiti mpana zaidi kuchunguza nafasi ya lugha mama katika mchakato wa ujipatiaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wajifunzaji warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2.

METHODOLOJIA

Utafiti katika makala hii ulifanyika katika vyuo vikuu viwili vya serikali ambavyo ni CKUB pamoja na CKB vilivyopo jijini Bujumbura. Katika makala hii ilitumika sampuli ya watoataarifa ishirini ambao walitoka katika vyuo viwili. Pia, katika kuteua sampuli yetu, mtafiti alitumia usampulishaji nasibu sahihi ambapo kila mtoataarifa alikuwa na haki sawa na mwingine. Watoataarifa walikuwa ni wanafunzi wanaosoma digrii mwaka wa tatushahada ya awali. Wanafunzi hao walihusika ili kuchunguza ukakamaaji wa matamshi unaojitokeza wanapojifunza Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi. Sababu za kuteua wanafunzi wa mwaka wa tatu ni kwamba tafiti tangulizi zinasema kuwa mwanafunzi wa Lg2 anakakamaa ikiwa angalau amejifunza miaka mitatu lugha hiyo (Bialystok na Miller, 1999). Aidha, wanafunzi wa vyuo vikuu hasa mwaka wa tatu walifaa kwa vile walikuwa wameanza kusoma lugha ya Kiswahili kuanzia shule ya msingi, shule ya upili, hadi Chuo Kikuu. Kawaida, mwanafunzi kama huyu anachukuliwa kuwa ana umilisi mwingi katika lugha. Hivyo, hatutarajii kuwa anaweza kukakamaa. Ndiyo maana mtafiti anaona amtathmini huyu wa Chuo Kikuu ili achunguze na ajue ikiwa wanafunzi wa Chuo Kikuu wanaweza kukakamaa au la. Katika makala hii ilitumika makabala wa kitaamuli ambao haswa ulihusisha maelezo zaidi kwa maana utafiti ulihusisha sana maelezo na mitazamo tu kuliko takwimu.

NADHARIA YA UTAFITI

Utafiti huu uliongozwa na Nadhariatete Teuzi ya Ukakamaaji (kuanzia sasa NATEU) ya Han (2009). Dai kuu la NATEU ni kuwa wajifunzaji wa Lg2 huchagua vipengele tu vya lugha fulani ambavyo hukakamaa kwavyo ila vingine hapana. Ina maana kuwa katika mchakato wa ujifunzaji Lg2, hushindwa kumudu vipengele fulani vya lugha kuliko vingine. NATEU ina mihimili mikuu miwili ambayo ni : Mosi, kuchunguza sababu za ukakamaaji kwa nduni za Lg2 na pili kueleza sababu za vipengele fulani vya kiisimu ambavyo hukakamaa haraka zaidi kuliko vingine. Pembeni na mihimili hiyo, Nadhariatete inadai kuwa kadri ya zana faafu, ufundishaji usio potovu, huo ukakamaaji unaweza kuondolewa kwa wajifunzaji. Nadharia hii ina kiolezo ambacho watafiti wa Lg2 hukitumia ili kubainisha vipengele ambavyo vinadhihirisha ukakamaaji kwa urahisi na vile ambavyo haviwezi kukakamaa kirahisi. Hivyo, kulingana na Nadhariatete hii inaweka vigezo vya kutumika kutathmini uwezo walionao wajifunzaji wa lugha kutumia lugha husika. Katika utafiti huu, itatusaidia kutumia lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia kanuni za Kiswahili sanifu. Pia, Nadhariatete hii inafaa katika makala yetu kwani mihimi yote miwili itatusaidia katika kujibu malengo yote ya utafiti kama inavyodhihirisha hapo awali. Mfano, msingi mkuu wa nadhariatete hii ni kwamba wajifunzaji wa Lg2 wanachagua vipengele ambavyo wanakakamaa. Makala yetu msingi huu ulitufaa kwani utafiti husika unahusu tu ambacho ni kipengele vya kifonolojia.

MATOKEO YA UTAFITI

Katika sehemu hii, mtafiti ameongelea fonimu kadha wa kadha zilizodhihirisha ukakamaaji kwa wajifunzaji Warundi waliokuwa wanasoma Kiswahili vyuo vikuu vya serikali Burundi. Fonimu hizo kama ilivyodhihirika kwa watoataarifa ni kama zifuatazo:

Ukakamaaji wa /ŋg/ badala ya /ŋ/

Data kutoka uwandani zilionesha kuwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2 wamekakamaa kwa baadhi ya vitamkwa kwenye vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi. Ukakamaaji huo mtafiti aligundua kwamba upo alipotumia mbinu ya masimulizi kwa watoa taarifa (wanafunzi) ambao amewapa zoezi la kusimulia hadithi kila mmoja aliokuwa ameteua. Walipokuwa wanasimulia hadithi kulijitokeza utamkaji wa sauti /ŋg/ ambayo ilisikika kwa imetumiwa vibaya. Hivyo, ni kumanisha kuwa badala ya kutamka sauti /ŋ/ kama ilivyokuwa inatakiwa walitumia mbadala wa sauti /ŋg/. Jambo lilionekana linasumbua wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu vya serikali Burundi. Mifano kadhaa ilibainishwa katika jedwali na. hapa chini.

Jedwali Na. 5.1: Ukakamaaji wa /ŋg/ badala ya /ŋ/

Namba	Matamshi yenye ukakamaaji		Matamshi sahihi	
	Mifano	Uwakilishi kifonetiki	Uwakilishi kiotografia	Uwakilishi kifoneti
1	ngombe	/ŋgɔmbɛ/	ng'ombe	/ŋɔmbɛ/
2	ngambo	/ŋgambɔ/	ng'ambo	/ŋambɔ/
3	akangangana	/akangangana/	akang'ang'ana	/akananana/
4	ngatuka	/ngatuka/	ng'atuka	/natuka/
5	ngata	/ngata/	ng'ata	/nata/
6	ngara	/ngara/	ng'ara	/nara/
7	ngoananga	/ngɔa nanga/	ng'oa nanga	/noa nanga/

Chanzo: Uwandani (2024)

Sambamba na data zilizowasilishwa hapo juu katika jedwali na.1.1 tunaona kuwa tatizo kubwa la ukakamaaji wa /ŋg/ badala ya /ŋ/ kwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2 katika vyuo

vikuu vya serikali Burundi linahusiana na tofauti za kimatamshi kati ya lugha ya nyumbani, za kimazingira, jamii inayowazunguka wajifunzaji na Kiswahili. Kwa Warundi, lugha ya Kirundi ambayo ni lugha asili kwao haina baadhi ya fonimu zinazopatikana katika Kiswahili, hususani zile za sauti kama /ɲ/. Hili linaweza kusababisha ugumu katika utamkaji wa fonimu hizo wanapojifunza au kutumia Kiswahili. Kutokana na maoni na mitazamo ya watoa taarifa waliosailiwa wakati wa ukusanyaji data, wanasema kuwa ukosefu wa fonimu katika lugha ya mama ni mojawapo ya vikwazo vinavyosababisha ukakamaaji huo. Ina maana kwamba lugha ya Kirundi ina mfumo tofauti wa sauti ukilinganisha na Kiswahili. Fonimu kama /ɲ/ haipo katika Kirundi, hivyo wazungumzaji wanaweza kutamka /ŋ/ badala ya /ɲ/ yake kutokana na kutozoa fonimu hiyo. Pia, kwa mujibu wa watoataarifa mazingira ya kujifunza lugha yanaweza kuzuia ujifunzaji mzuri wa lugha ya Kiswahili.

Kwa uhalisia kwamba Warundi wanajifunza Kiswahili kama Lg2, inawezekana mafunzo hayajazingatia mazoezi ya kina hasa ya sauti, wanafunzi hujenga mazoezi ya matamshi yasiyo sahihi. Aidha, ushawinshi wa lugha ya kwanza kuwa mkubwa kwa watu wanapojaribu kutamka fonimu za Kiswahili. Ina maana fonolojia ya lugha ya kwanza inakuwa msingi, na inapoingiliana na lugha ya pili, matokeo huwa ni mwingiliano wa kifonolojia. Ndipo kunaibuka ukakamaaji wa wajifunzaji hao. Isitoshe, kuna wajifunzaji ambao wanakuwa na ukosefu wa maarifa kuhusiana na tofauti ndogo za kifonolojia kwa maana wengi huona kuwa tofauti kati ya /ŋ/ na /s/ ni ndogo. Hivyo, kutozingatia tofauti hiyo inavyopaswa ikasababisha ujifunzaji mbaya hadi kukakamaa. Hii ni changamoto ya kawaida kwa wazungumzaji wa lugha ya pili ambao hawana mafunzo ya kina ya sauti.

Ukakamaaji wa Sauti /s/ badala /θ/

Fonimu hii /θ/ ni kikwamizi na si sauti ya meno. Ina maana hutamkwa wakati ncha ya ulimi inaweka katikati ya meno ya juu na ya chini. Katika utamkaji wa sauti hii, badala ya mkondohewa kubanwa kabisa, huachiwa kupita lakini kwa kugusanisha alasogezi na alatuli kiasi kwamba sauti hutoka kwa kukwamakwama. Sauti /θ/ ilisikika kupotoshwa sana kwa watoa taarifa wanafunzi walipokuwa wanahadithia wakati walikuwa wanampa data mtafiti. Takribani watoa taarifa wote walipokuwa wanafika kwenye sauti hii iliwashinda kutamka na kuifaninisha na /s/ kama ilivyobaishwa hapo chini kwenye jedwali.

Jedwali Na. 5.2 : Namna Watoataarifa walivyokakamaa kwaSauti /s/ badala /θ/

Na.	Matamshi yenye ukakamaaji		Matamshi sahihi	
	Mifano	Uwakilishi kifonetiki	Uwakilishi kiotografia	Uwakilishi kifoneti
1	Selasini	/selasini/	thelathini	/θɛla'θi:ni/
2	semanini	/semanini/	themanini	/θɛma'ni/
3	sumuni	/sumuni/	thumuni	/θu'mu:ni/
4	selusi	/selusi/	theluthi	/θɛ'luθi/
5	semometa	/semometa/	themometa	/θɛmɔ'meta/
6	seluji	/seluji/	theluji	/θɛ'luji/

Chanzo: Uwandani (2024)

Kama ilivyobainika katika jedwali na.1.2kwamba wajifunzaji vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi wanapohidithia wamekakamaa hasa katika kubali kitamkwa kimoja badala ya kingine mathalani ni utamkaji wa sauti /s/ badala ya /θ/. Hali hii mtafiti pamoja na watoa taarifa aliowasili wanaona kuwa kwanza kabisa ni kuwa lugha ya Kirundi (Lg1) inakosa sauti mbalimbali ambazo zinapatikana katika lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha lengwa. Sababu ya kutokuwa na sauti hiyo inayotamkwa katika kugusana kati ya meno na ulimi /θ/,

wazungumzaji Warundi wakati wa kutamka wanaweza kutumia sauti /s/ ambayo sasa ni rahisi zaidi na iko karibu katika eneo la utamkaji. Pili, watoa taarifa walidai kuwa hata ushawinshi wa matamshi ya Lg1 yaweza kuchangia kwa namna Fulani kwa maana sauti hiyo haipo katika Kirundi. Kingine kinachowezezana kusababisha ukakamaaji huo kwa hawa wajifunzaji ni uhamishaji wa lugha ambapo wanafanya uhamishaji wa sauti kutoka Lg1 kwenda Lg2 ambayo ni lengwa. Hayo yote yanatokana na kwamba Lg1 haina sauti /θ/. Vilevile sauti hizo mbili zina sifa jumuishi wa matamshi ambayo ni sambamba kwa vitamkwa vyote viwili. Kitamkwa /s/ni kikwamizi sikhuna cha ufizi. Fonimu zote mbili zipo katika daraja moja, yaani jinsi ya matamshi.

Aidha, katika usaili tuliofanya na wahadhiri vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi, mtafiti alitaka kujua kuwa katika lugha ya Kirundi kuna maneno ambayo yana sauti /θ/. Majibu ambayo wametoa wahadhiri hao yanatuonesha kuwa katika Kirundi hakuna sauti /θ/ na kinyume chake kuna kitamkwa /s/. Shida hii ya ukosekanaji wa sauti /θ/ ipo kwenye makabila mengi ya kibantu ambayo yanapatikana katika ukanda wa ziwa victoria, kwani hata mtalaamu Wenceslaus (2015) katika kabila la Kijita ambalo nalo linapatikana katika ukanda wa ziwa victoria alikutana na tatizo hilo. Kuhusiana na utafiti wa sasa, mtafiti aligundua kuwa wajifunzaji Warundi vyuo vikuu vya serikali huwa wanashindwa kutofautisha vitamkwa /s/ na /θ/ wanapohadithia darasani. Kitamkwa /θ/ ni kikwamizi lakini pia ni kitamkwa ambacho hutamkiwa kwenye meno, kitamkwa /s/ hii hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapowekwa katikati ya meno ya juu na ya chini. Ili kuitamka sauti hii kwa ufasaha, ni lazima kubana mkondohewa kabisa na kuiachia kupita ingawa kwa kugusanisha kidogo alasogezi na alatuli kiasi cha kuifanya sauti kutoka kwa kukwamakwama.

Ukakamaaji wa Kuchopeka Kiyeyusho /w/

Kama Massamba (2009) anavyoeleza kuwa uchopekaji ni uingizaji wa irabu, kiyeyusho au konsonanti katika neno, basi kwa maelezo sahihi tunaweza kusema kuwa uchopekaji ni kama hali ambapo kitamkwa kinaingizwa katikati ya mfululizo wa vitamkwa vingine ambavyo vipo tayari katika neno. Hivyo, mfanyiko kama huu unasaidia lugha kuoanisha matamshi ya maneno na mfumo wa kifonolojia, hasa, kwa kuzingatia misingi ya silabi za lugha husika. Aghalabu, vitamkwa vinavyochopekwa vinaweza wakati mwingine kuwa na manufaa au visiwe na manufaa, hasa hasa pale ambapo misingi ya mfanyiko huu huwa una asili katika lugha ya kwanza. Tazimili hii inathibitisha kuwa wajifunzaji Warundi katika vyuo vikuu vya serikali wamekakamaa walipofanya ukakamaaji wa uchopekaji wa kiyeyusho /w/. Maneno yaliyojitokeza kuwa yamechopeka kiyeyusho hicho ni kama vile: mwoyo badala ya moyo, nguwo badala ya nguo, ndowa badala ya ndoa, wawo badala ya wao.

Jedwali Na .5.3: Uchopekaji wa kiyeyusho /w/ mahala kisipotakiwa

Na.	Matamshi yenye ukakamaaji		Matamshi sahihi
	Uwakilishi kiotografia		Uwakilishi kiotografia
1	nguwo		nguo
2	ndowa		ndoa
3	wawo		wao
4	mwoyo		moyo
5	nahuli		nauli
6	Sina*akika		Sina hakika
7	Baba yake Mzee mashaka akaahidi	atawoga mwaka	Baba yake Mzee mashaka akaahidi ataoga mwaka ujao ujawo

Chanzo: Uwandani (2024)

Kutokana na data kutoka uwandani ni dhahiri kuwa Wajifunzaji Warundi vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi wamekakamaa kimatamshi. Kama ilivyobainishwa katika jedwali Na. 5.3 hapo awali ni kwamba wajifunzaji wa Kiswahili kama Lg2 nchini Burundi wamedhihirika kukakamaa kwa baadhi ya fonimu za Kiswahili kama lugha lengwa. Baadhi ya ukakamaaji huo mojawapo ni huku walipokuumbwa na uchopekaji wa kiyeyusho /w/ pamoja /h/ kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili wakati walisimulia hadithi. Aidha, katika kugundua uhalisia kuwa wajifunzaji Warundi wamekakamaa nasdhariatete Teuzi ya Ukakamaaji (Han, 2009) ilitusaidia kwa maana dai kuwa la nadhariatete ni kuwa wajifunzaji wa Lg2 ama ya kigeni huwa wanakakamaa kwenye karibu vipengele vyote vya kiisimu tukianza fonolojia hadi vilongo. Tukijikita kwa data kutoka kwa Wahadhira vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi ni kwamba hali hii inasababishwa na miundo ya silabi ya Kirundi ambayo haikubali kuwa funge badala yake inapenda kuwa wazi tofauti na lugha ya Kiswahili. Hivyo, wanapojifunza hukumbwa na uchopekaji wa kiyeyusho /w/ na sauti /h/ kwa baadhi ya maneno kimatamshi.

Ukakamaaji waSauti /ð/ kuwa/θ/

Kutokana na data kutoka kwa watoataarifa (wanafunzi) ambao katika masimulizi yao ya hadithi wamekakamaa katika baadhi ya fonimu za Kiswahili, lugha lengwa waliyokuwa wanajifunza ikiwa Lg2 vyuo vikuu vya serikali Burundi. Mtafiti amebaini mwisho kuwa pamoja na kwamba Lg1 kwa wajifunzaji Warundi hakuna sauti za vikwamizo vya meno /ð/ na /θ/walijitokeza wazungumzaji Warundi walioshindwa kabisa kutamka na hatimaye kutofautisha sauti hizi wanapotamka Kiswahili sanifu darasani. Baada ya mtafiti kusikiliza mara kadhaa sauti za watoa taarifa (wanafunzi) alizonasa, hakika aligundua matamshi ya fonimu yenye kudhihirisha ukakamaaji kwa wajifunzaji Warundi katika vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi. Kama alivyoonesha katika Jedwali Na. 5.4 hapo chini.

Jedwali Na.5.4: Ukakamaaji wa Sauti /ð/ kuwa/θ/

Na.	Mifano yenye ukakamaaji	Uwakilishi kifonetiki	Maneno yenye Kiswahili sanifu	Uwakilishi kifoneti
1	wakathoofisha	/wakaθɔɔ'fiʃa/	wakadhooofisha	/wakaðɔɔ'fiʃa/
2	Ilikuwa ni thambi katika jamii hiyo..	/l'θambi/	Ilikuwa ni dhambi katika jamii hiyo	/l'ðambi/
3	Ikawa adhari kwa jamii...	/a'ðari/	Ikawa athari kwa jamii	/a'θari/
4	Mtoto huyo alikuwa na dhamani sana.	/ða'mana/	Mtoto huyo alikuwa na thamani sana	/θa'ma:ni/
5	Wakati huo huo thoruba ikasikika	/θɔ'ruba/	Wakati huo huo dhoruba ikasikika	/ðɔ'ruba/
6	Akaja kijana dhabiti	/ða'biti/	Akaja kijana thabiti	/θa'biti/
7	Hali ilikuwa dhakala sana	/ða'kala/	Hali ilikuwa thakala sana	/θa'kala/

Chanzo: Uwandani (2024)

Ni dhahiri kwamba data kutoka uwandani kama zilivyowasilishwa katika jedwali Na.5.4 Zilithibitisha kuwa ukakamaaji uliotokana na ufundishaji potofu kwa wajifunzaji Warundi vyuo vikuu Burundi. Hoja hiyo ilitoka kwa baadhi ya watoataarifa (wahadhiri) katika vyuo vikuu hivyo vya serikali Burundi kuwa kuna baadhi ya Walimu hasa wale waliofundisha wajifunzaji hao katika ngazi za sekondari walioshindwa kuwafundisha wanafunzi hao hadi kubaki na matamshi yasiyofaa ya vitamkwa hivyo. Jambo ambalo hadi sasa vyuo vikuu linawasababishia kukakamaa wanapozungumza lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, sauti /ð/ na /θ/zina mfanano wa karibu ambapo zote mbili hutamkiwa kwenye meno (mahala pa matamshi) na vilevile tukizungumzia jinsi ya matamshi sauti zote mbili ni vikwamizo ijapokuwa tu sauti /dh/ inakuwa sauti ghuna ilhali sauti /θ/si ghuna. Hivyo, mjiifunzaji anapotumia sauti mojawapo badala ya nyenzake, sababu kubwa ni ule mfanano wa sifa zake za kifonetiki.

Kadhalika, matumizi hayo mbadala kwa Warundi yanaelekea kuwa yamesababishwa na ukosefu wa mazoea ya kutumia maneno hayo katika lugha ya Kirundi. Kwa mfano maneno kama dhoruba, thamani, dhambi yana silabi kama \$dho\$, \$tha\$, \$dha\$ hazipo kamwe katika muundo wa silabi za Kirundi. Kwa hiyo, kwa kuwa huo unakuwa mtindo mpya wa lugha kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi; hali hiyo inahusiana na mawazo yaliyowahi kutolewa na wataalamu wengine kama vile Perdue (1993), Preston (1989), Schumann (1978a) na Stauble (1978) kwamba, kukakamaa kwa wajifunzaji wa Lg2 kunasababishwa na wajifunzaji wa Lg2 kutojua vizuri lugha husika wayojifunza.

Ukakamaaji wa kundoshasha sauti /h/ mwanzoni mwa neno

Udondoshaji kama utaratibu wa utoaji wa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au kishazi (Massambam, 2009).Udondoshaji ni mchakato wunaohusu uachaji wa baadhi ya vitamkwa katika utamkaji wa maneno ya lugha. Naye Massamba (2011) anaeleza kuwaudondoshaji wa sauti katika lugha unaweza kutokea mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno. Kwa mujibu wa maelezo haya tazimili hii ilichunguza ukakamaaji wa kimatamshi kwa wajifunzaji wa Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu nchini Burundi ambapo baada ya watoa taarifa kuhadhifia mmoja baada ya mwingine mtafiti aligundua kuwa baadhi ya wajifunzaji wafanya udondoshaji wa fonimu wanapojifunza Kiswahili. Kama itakavyoelezwa katika zilizofuata mifano itaeleza barabara jambo.

Jedwali Na.5.5 linaonesha wazi ukakamaaji mwingine unaoathiri wajifunzaji Warundi katika mchakato wa kujifunza Kiswahili kama Lg2. Ukakamaaji huu huwa unatokea pale wazungumzaji wa Lg1 wanapopunguza viambishi vya awali ambavyo vinasimama kama mzizi wa maneno hayo husika. Aidha, wazungumzaji hao wa lugha ya Kiswahili wanaoathiriwa na lugha ya Kirundi huwa wanapunguza viambishi wakati wanapozungumza Kiswahili, lengo lao ni moja tu la kukidhi mazungumzo ila wakasahau kuwa kuna sharia na kanuni za lugha ya Kiswahili. Kwa ufupi, kutokana na data za uwandani utafiti huu ulibaini kuwa Warundi wanapoongea huwa wanapunguza vitamkwa katika maneno ya Kiswahili kama ilivyobainika kwa wajifunzaji Warundi katika vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi.

Ili kuwa bayana ibainike kuwa katika utafiti huu maneno yaliyofanyiwa utafiti na kuonekana kuwa yanawasababishia ukakamaaji wanafunzi wa darasa la tatu vyyo vikuu viwili vya serikali nchini Burundi ni baadhi ya maneno ya Kiswahili yanayoanza na sauti /h/ ambapo kwa wanafunzi wengi wakati wanasimulia hadithi unawasikia wakitamka wakidondosha kitamkwa /h/. Mathalani ya maneno hayo ni kama "hapana" wanasikika wakitamka "apana", neno "hatari" wanalitamka "atari", neno "hamsini" wanalitamka "amsini" na mengine kama yalivyoorodheshwa katika Jedwali Na.4

Jedwali Na .5.5: Ukakamaaji wa kudondosha kitamkwa /h/ mwanzoni mwa neno

Namba	Matamshi yenye ukakamaaji		Matamshi sahihi	
	Mifano	Uwakilishi kifonetiki	Uwakilishi kiografia	Uwakilishi kifoneti
1	amna	/a'mna/	hamna	/ha'mna/
2	amusini	/am'si:ni/	hamsini	/ham'si:ni/
3	apana	/a'pa:na/	hapana	/ha'pa:na/
4	atari	/a'ta:ri/	hatari	/ha'ta:ri/
5	alafu	/a'lafu/	halafu	/ha'lafu/
6	odari	/o'dari/	hodari	/o'dari/

Chanzo: Uwandani (2024)

Udondoshaji ni hali ya kudondoa kipashio katika neno kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika. Habwe na Karanja (2007) wanasema kwamba, mfanyiko huu unahusu kuachwa nje kwa sauti fulani ya neno ili kuoanisha matamshi yake. Tofauti katika utaratibu wa mfuatano wa sauti katika uundaji wa maneno kati ya lugha ya Kirundi (Lg1) pamoja na Kiswahili (Lg2) zilisababisha kudondoshwa kwa sauti /h/ kwa njia iliyoleta kasoro katika maneno mbalimbali.

Kama inavyosomeka katika Jedwali Na.5.5 hapo juu kutoka uwandani pembeni na ushahidi kutoka kwa wajifunzajilugha wenye walivyotamka katika masimulizi yao ya hadithi darasani kuwa huu udondoshaji wa kitamka /h/ katika mifano hiyo ina maana kuwa, hakuna fonimu yoyote katika mazingira ambapo kimsingi ilitakiwa kuwapo kwa mujibu wa utaratibu wa Kiswahili sanifu. Hivyo, ikumbukwe kuwa utafiti ulifanya uchunguzi kuhusu ukakamaaji kimatamshi ambao ulionekana wa aina nyingi ikiwamo hii ya udondoshaji wa fonimu /h/ kama ilivyobainika katika jedwali Na.5.5 hali ya kudondosha fonimu ni kuitoa kabisa hiyo katika mazingira ya umbo la nje la neno bila kuwa na fonimu nyingine ya kuichukua nafasi iliyoachwa. Uchunguzi uliofanywa kwa watoataarifa (wanafunzi) kwenye vyyo vikuu vya serikali Burundi, umethibitisha kuwa fonimu ya kikwamizi /h/ hudondoshwa na watoataarifa katika baadhi ya maneno ambayo ni lazima fonimu isikike wanapongea.

Ukakamaaji wa Sauti /s/ kutamkwa kama /ʃ/ na kinyume chake

Kama ilivyobainishwa katika jedwali Na.5.6 kulisikika ukakamaaji wa sauti /s/ kutamkwa kama /ʃ/ wakati wa ukusanyaji wa data. Utafiti umegundua kuwa wajifunzaji Warundi katika vyyo vikuu viwili vya serikali ambavyo vilikuwa ni Chuo Kikuu cha Burundi (CHB); hususani Idara ya Kirundi na Kiswahili pamoja na Chuo Kikuu cha Uallimu cha Burundi (CHUB) katika idara ya Kirundi-Kiswahili wanatamka sauti /s/ badala ya /ʃ/ wanaposimulia hadithi. Wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa Kirundi kama lugha yao ya Kwanza hutamka sauti /s/ katika maneno ya Kiswahili yenye sauti /ʃ/.

Utafiti huu umebaini na kugundua kuwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili ikiwa ni lugha yao ya pili wanakosea katika kutamka baadhi ya sauti sababu katika lugha yao ya kwanza kuna sauti kama hii /ʃ/ inapatikana katika lugha ya Kirundi. Hivyo, kutokana na ukaribu huo kuwa sauti ipo wajifunzaji wanajumuisha na kuitamka vilevile ilivyo katika Kirundi kwenye Kiswahili ilhali maana inapotoshwa na kujikuta wamekakamaa. Mathalani ya maneno ya Kirundi ambayo yana sauti /ʃ/ ni kama inavyosomeka katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na.5.6:Mifano ya Maneno katika Kirundi yanayoanza na /ʃ/

Na.	Maneno ya Kirundi yenye sauti /ʃ/	Kiswahili chake
1	Shiramwo	tia
2	shikira	chukua
3	shika	pokea
4	shigikira	Unga mkono, tetea
5	shishikara	Endelea, songa mbele, piga hatua
6	shinga	weka
7	shaza	pendeza
8	shogomanga	tembea bila wasiwasi
9	shima	shukuru
10	Shimangira	shadidia

Kama ilivyobainika hapo juu katika Jedwali Na.5.6 ni kwamba katika lugha ya Kirundi kuna baadhi ya maneno yanayoanza na sauti /ʃ/ ambayo pia inapatikana katika lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, baadhi ya wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili katika vyyo vikuu vya serikali nchini Burundi wanachua matamshi yale wanayoyazoea katika lugha yao ya kwanza na kuyatumia vilevile katika Kiswahili. Jambo ambalo linawasababishia kukakamaa kwa fonimu hizo ambazo wanazichukua kama za lugha yao tu ilahali ni lugha ya Kiswahili.

Kama ilivyobainika hapo juu katika Jedwali Na.5.6 ni kwamba katika lugha ya Kirundi kuna baadhi ya maneno yanayoanza na sauti /ʃ/ ambayo pia inapatikana katika lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, baadhi ya wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili katika vyyo vikuu vya serikali nchini Burundi wanachua matamshi yale wanayoyazoea katika lugha yao ya kwanza na kuyatumia vilevile katika Kiswahili. Jambo ambalo linawasababishia kukakamaa kwa fonimu hizo ambazo wanazichukua kama za lugha yao tu ilahali ni lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na. 5.7 : Ukakamaaji wa Sauti /s/ kutamkwa kama /ʃ/ au kinyume

Na.	Matamshi yenye ukakamaaji		Matamshi sahihi	
	Mifano	Uwakilishi kifonetiki	Uwakilishi kiortografia	Uwakilishi kifoneti
1	shimama	/ʃimama/	simama	/simama/
2	shindikiza	/ʃindikiza/	sindikiza	/sindikiza/
3	sika	/sika/	shika	/ʃika/
4	serehekea	/serehekea/	sherehekea	/ʃerehekea/
5	shimama	/ʃimama/	simama	/si'mama/

Chanzo: Uwandani (2024)

Ukakamaaji wa Sauti /d/ badala ya /ð/

Fonimu hii ni kikwamizi lakini pia ni sauti ya meno. Ina maana hutamkwa wakati ncha ya ulimi inawekwa katikati ya meno ya juu na ya chini. Katika utamkaji wa sauti hii, badala ya mkondohewa kubanwa kabisa, huachiwa kupita lakini kugusanisha alasogezi na alatuli halafu sauti hutoka kwa kukwamakwama. Katika mchakato wa ujifunzaji wajifunzaji Warundi hushindwa kutofautisha sauti /d/ na /ð/. Ilihahirika wakati wa ukusanyaji wa data ambapo wajifunzaji wakati wa usimulaji hadithi walishindwa kutamka sauti /ð/ badala yake wakatamka sauti /d/. Aidha, kimsingi fonimu /d/ na /ð/ ni fonimu tofauti. Sifa zake bainifu za utamkaji, usikivu na mahali pa kutamkia zinadhahirisha tofauti baina yake. Pamoja na tofauti zilizo, wajifunzaji Warundi wakati wanasimulia hadithi huwa wanashindwa kutofautisha sauti hizo mbili na kukakamaa. Taz. Jedwali hapa chini ili kuona namna walivyokakamaa kwenye baadhi ya sauti za Kiswahili sanifu.

Jedwali Na.5.8 : Ukakamaaji wa Sauti /d/ badala ya /ð/

Na.	Matamshi yenye ukakamaaji		Matamshi sahihi	
	Mifano	Uwakilishi kifonetiki	Uwakilishi kiortografia	Uwakilishi kifoneti
1	dambi	/ 'dambi /	dhambi	/ 'ðambi /
2	dahabu	/ 'dahabu/	dhahabu	/ 'ðahabu/
3	mhadi	/mha'diri/	mhadi	/mha'ðiri/
4	hadira	/ha'dira/	dhadi	/ha'ðira/
5	nakadalika	/nakada'lika/	nakadhalika	/nakaða'lika/
6	taadima	/ta: 'dima/	taadhima	/ta: 'ðima/
7	ninadani	/nina'da:ni/	ninadhani	/nina'ða:ni/
8	maudui	/mau'duwi/	maudhui	/mau'ðuwi/
9	madumuni	/madu'mu:ni/	madhumuni	/maðu'mu:ni/
10	shukrani za dati	/ʃu'krani za dati/	Shukrani za dhati	/ʃu'krani za ðati/
11	bidaa	/bi'daa/	bidhaa	/bi'ðaa/
12	Kijana kaombwa adabu	/a'dabu/	Kijana kaombwa adhabu	/a'ðabu/
13	Kijana mwenye udaifu wa kufanya kazi	/uda'jifu/	Kijana mwenye udhaifu wa kufanya kazi	/uða'jifu/
14	Dairi	/da'hiri/	dhahiri	/ða'hiri/
15	Baba alikuwa anadabihi mnyama ili kupata mali nyingi	/anadabihi/	Baba alikuwa anadhabihi mnyama ili kupata mali nyingi	/anaðabihi/
16	Kijitu kikawadibiti njiani	/kikawadi'biti/	Kijitu kikawadhibiti njiani	/kikawaði'biti/
17	Alikuwa anajikinga didi ya.....	/didi/	Alikuwa anajikinga dhidi ya.....	/ðidi/
18	Akamdihaki	/akamdi'ha:ki/	Akamdihaki	/akamði'ha:ki/
19	Msichana akaja kudihirika mjamzito..	/kudihiri'rika/	Msichana akaja kudihirika mjamzito..	/kuðihiri'rika/
20	Askari akawa dhuli....	/duli/	Askari akawa dhuli....	/ðuli/

Chanzo: Uwandani (2024)

Wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu Burundi hutatizwa sana kimatamshi wanapotamka baadhi ya konsonanti za Kiswahili kama /ð/ ambayo ilisikika kutamkwa /d/ wanaposimulia hadithi. Ifahamike kwamba lugha ya Kirundi ambayo ni lugha mama kwao haina sauti /ð/. Hivyo, ukosefu ama kutokuwa na konsonanti hiyo katika Lg1 kwa wanafunzi hawa kunaibuakizuizi cha utamkaji faafu wa sauti hiyo katika Kiswahili. Kutokana na sababu hizo badala ya kutamka konsonanti hiyo wajifunzaji Warundi huamua kutumia konsonanti ambayo inaweza kupatikana katika Lg1 mahala pa konsonanti /ð/ ya Lg2.

Ukakamaaji wa Sauti /g/ badala ya /ɣ/

Lugha ya Kirundi ina sauti amnbazo huwezi kupata kama kama ilivyo katika lugha nyingine lakini pia kama ilivyobainika wakati wajifunzaji Warundi vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi walipokuwa wanahadithia. Hali hii ilijitokeza kwa wanafunzi wa mwaka wa tatu CKUB pamoja na CKB katika idara zinazofundisha Kirundi na Kiswahili. Wajifunzaji hao walishindwa kutamka sauti /ɣ/. Badala yakewalitamka sauti /g/. Ukakamaaji huo unaonekana kwa hao wajifunzaji Warundi unathibitishwa kwa asilimia kubwa na watoataarifa (wahadhiri vyuo vikuu) na kusema kwamba sababu kuu ni kuwa katika Lg1 ya hao wajifunzajilugha hawana sauti /ɣ/. Jambo linalozua utata zaidi na kuwasababishia kukakamaa wanapotamka sauti hiyo wakati wanajifunza Kiswahili ikiwa lugha yao ya pili. Hapa chini ni mifano kadhaa inayoweka bayana namna wajifunzaji walivyokakamaa kwa baadhi ya sauti za Kiswahili wakati wanasimulia hadithi.

Jedwali Na.5.9: Ukakamaaji wa Sauti /g/ badala ya /ɣ/

Na.	Matamshi yenye ukakamaaji		Matamshi sahihi	
	Mifano	Uwakilishi kifonetiki	Uwakilishi kiotografia	Uwakilishi kifoneti
1	shuguli	/ʃuˈguli/	shuguli	/ʃuˈɣuli/
2	gala	/ˈgala/	gala	/ˈɣala/
3	gafla	/ˈgafla/	gafla	/ˈɣafla/
4	gadhabu	/gaˈða:bu/	ghadhabu	/ɣaˈða:bu/
5	gafi	/ˈga:fi/	ghafi	/ˈɣa:fi/
6	lagai	/laˈgaji/	laghai	/laˈɣaji/
7	gasia	/gaˈsia/	ghasia	/ɣaˈsia/
8	gashashi	/gaˈʃaʃi/	ghashashi	/ɣaˈʃaʃi/
9	gashi	/ˈgaʃi/	ghashi	/ˈɣaʃi/
10	garama	/gaˈrama/	gharama	/ɣaˈrama/
11	luga	/ˈlu:ɣa/	lugha	/ˈlu:ɣa/
12	gali	/ˈgali/	ghali	/ˈɣali/
13	gafilika	/gaˈfili/	ghafilika	/ɣaˈfili/
14	gafuri	/gaˈfuri/	ghafuri	/ɣaˈfuri/
15	gamu	/ˈgamu/	ghamu	/ˈɣamu/

Chanzo: Uwandani (2024)

Kama ilivyobainika katika jedwali Na.5.9 wajifunzaji Warundi katika mchakato wa kujifunza Kiswahili kama Lg2 wamekakamaa kwa baadhi ya vitamkwa. Mathalani ni kikwamizo cha kaakaa laini /gh/ ambacho hakipatikani katika mfumo wa lugha ya Kirundi ambayo wajifunzaji wanayozungumza kama Lg1 kwao. Hivyo, wanapohadithia wao huwa wanarahisisha mambo na kutumia kipasuo ambacho ni ghuna /g/. Ijulikane kuwa katika lugha ya Kirundi kipasuo ghuna /g/ kinapatikana katika mfumo wa sauti lakini pia kinapatikana katika Kiswahili sanifu. Hivyo, wajifunzaji wamechukua rahisi maneno yenye kaakaa laini /ɣ/ na kuitamka kama /g/ ili wasitatizike. Hali kama hii ilichangia kwa wajifunzaji Warundi kukakamaa kimatamshi wanapotamka vitamkwa hivyo katika Kiswahili sanifu. Isitoshe, sauti /g/ na /ɣ/ zote hutamkiwa kwenye sehemu moja ya kinywa kwani ni kaakaa laini ingawa moja ni kipasuo /g/ ilhali nyingine ni kikwamizo. Maana hupotea zinapotumiwa mbadala wanapotamka. Hata hivyo, maana wakati mwingine hupotea hasa hasa anayezungumza akiwa anaelewa jinsi mjifunzaji wa Kiswahili amehamisha mfumo wa sauti za Lg1 ambayo ni lugha mama kwake.

Ukakamaaji wa Kuchopeka Sauti /h/

Wajifunzaji wa Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu vya serikali Burundi walipokuwa wanahadithia darasani walichopeka kiholela sauti ambayo ni konsonanti /h/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Aidha, konsonanti /h/ imo katika mfumo wa Lg1 ambayo ni Kirundi pamoja na lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na.5. 10: Ukakamaaji wa Kuchopeka Sauti /h/

Na.	Mifano	Uwakilishi kifonetiki	Uwakilishi kiotografia	Uwakilishi kifoneti
1	Wakati ulee habiria wakajaa kwenye kituo	/habɪˈrɪja/.....	Wakati ulee abiria wakajaa kwenye kituo	/abɪˈrɪja/.....
2	Mzee huyo walikuwa wanapendana hawali ila.....	/haˈwali/.....	Mzee huyo walikuwa wanapendana awali ila.....	/haˈwali/.....
3	Mwishowe rahia wakaja kupiga kura.....	/raˈhɪja/.....	Mwishowe raia wakaja kupiga kura.....	/raˈhɪja/.....
4	Mahali hapo sitahasahau	/sitahasahau/.....	Mahali hapo sitapasahau	/sitapasahau/.....
5	Wakati huo akahafika salama	/akahaˈfika/.....	Wakati huo akapafika salama	/akapaˈfik/.....

Chanzo: Uwandani (2024)

Kwa uzingativu wa mifano iliyobainishwa katika jedwali hapo juu lenye Na.5.10 ni dhahiri shahiri kwamba wajifunzaji wa Kiswahili wanaozungumza lugha ya Kirundi huwa wanachopeka sauti /h/ katika maneno ya Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa Guthrie (1948: 37), lugha za Kibantu nyingi zina mfanano kwa baadhi ya sauti au muundo wake. Hivyo, tukaweza kusema kwa kuwa Kirundi na Kiswahili ni lugha za Kibantu zote mbili zina sauti /h/. Hivyo, kwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu vya serikali, sauti hiyo si ngeni kwao. Uchopekaji wa sauti hii katika maneno ya Kiswahili kwa wajifunzaji Warundi wanaozungumza Kirundi kama Lg1 umedhihirika wakati wa usimulaji hadithi darasani. Aidha, Masebo na Nyangwine (2008: 91), wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za Kibantu. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni ya pili katika jamii nyingi za Kibantu, athari ya Lg1 inaonekana sana katika matamshi. Vilevile, lugha za Kibantu zimeathiri lugha ya Kiswahili katika maana, msamiati na sarufi. Katika utafiti wetu tumeshughulikia tu matamshi. Mara nyingi uchopekaji wa sauti /h/ mwanzoni mwa maneno ya Kiswahili ambayo yanaanza na vokali husababishwa na matamshi ya wazungumzaji wazawa walio wengi wa lugha ya Kirundi. Hitilafu hiyo ndiyo iliyotokea wakati watoataarifa walipokuwa wanasimulia hadithi darasani. Isitoshe, kwa vile walikuwa ni wajifunzaji wa vyuo vikuu ambao wamejifunza Kiswahili kuanzia shule ya msingi hadi chuo wamechukuliwa kuwa wamekakamaa.

Ukakamaaji huo umekuwa ukidaiwa na wataalamu wengi wakiwamo Bialystok na Miller (1999) wanafafanua zaidi kuwa wajifunzaji wa Lg2 au ya kigeni wanapojifunza takribani miaka mitatu na hatimaye wakaendelea kukakamaa kwa kutamka fonimu mbalimbali, fonimu hizo zinaimarika na kuwa sugu. Hii ina maana kuwa wajifunzaji Warundi ni bayana kuwa walikuwa wamejifunza lugha ya Kiswahili miaka mingi zaidi ya mitatu kwa kuwa hawangeweza kufika Chuo Kikuu kabla hawajasoma Kiswahili. Hivyo, wajifunzaji kama hao wanachukuliwa kuwa wana msingi wa lugha kwa maana kuwa hatua ya Chuo si jambo la kupuuzia. Ndipo sasa baada ya kukuta wanatamka baadhi ya sauti za Kiswahili isivyo na kuhakiki mitazamo ya watoataarifa walioshiriki katika kazi hii mtafiti ameamua kuthibitisha kuwa wajifunzaji Warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2 wamekakamaa.

Ukakamaaji wa Kuchopeka Sauti /u/ na /i/ katika silabi funge

Mtalaamu Matinde (2012: 134) anasema kuwa silabi funge ni silabi ambazo huishia kwa konsonanti. Hivyo, katika lugha ya Kiswahili ni dhahiri shahiri kuwa kuna maneno yenye silabi funge ambapo mtafiti amegundua kuwa baadhi ya wanafunzi huwa wanachopeka irabu au vokali /i/ au /u/ katika silabi funge za Kiswahili kilicho nasifu. Utafiti huu unahusu ukakamaaji wa kimatamshi kwa Warundi wanaojifunza Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu nchini Burundi. Kama nadhariatete Teuzi ya Ukakamaaji (Han, 2009) inavyodai ni kwamba wanafunzi wamekakamaa kwenye baadhi ya kutamka fonimu mbalimbali kama ilivyobainishwa hata katika majedwali kadhaa katika aya zilizotangulia na zitakazokuja mbele.

Sababu zinazosababisha wajifunzaji Warundi kukakamaa ni nyingi na tofauti ila hapa kwenye uchopekaji huu wa irabu hizo tunaweza kuthibitisha kuwa wazungumzaji Warundi (Lg1) huwa husikika kuchopeka /u/ na /i/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu yenye muundo wa silabi funge. Hivyo, ni kutokana na ile hali kwamba Kirundi na Kiswahili zilijulikana kama lugha ambishi bainishi; aghalabu lugha hizo zinakuwa na muundo wa silabi zilizo wazi. Hata hivyo, lughaya Kiswahili huwa na silabi funge hususani katika maneno yenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Mathalani ni maneno daktari, labda, daftari, n.k (Iribemwangi, 2010). Mtafiti ameonesha katika jedwali hapa chini ili kusaidia kutambua ni maneno gani Warundi wanakakamaa wanapozungumza lugha ya Kiswahili.

Jedwali na.5.11: Ukakamaaji wa kuchopeka Sauti /u/ na /i/ katika silabi funge

Na.	Matamshi ukakamaaji yenye		Matamshi sahihi	
	Mifano	Uwakilishi kifonetiki	Uwakilishi kiotografia	Uwakilishi kifoneti
1	daktari	/dakita:ri/	daktari	/dak'ta:ri/
2	labuda	/labuda/	labda	/labda/
3	elufu	/elufu/	elfu	/elfu/
4	afrika	/a:frika/	afrika	/a:'frika/
5	dafutari	/dafutari/	daftari	/daft'ari/
6	makataba	/maka'taba/	maktaba	/mak'taba/

Chanzo: Uwandani (2024)

Ni dhahiri shahiri katika jedwali kuwa wanafunzi katika vyuo vikuu vya serikali Burundi wamekakamaa kwenye baadhi ya fonimu walipokuwa wanajifunza Kiswahili kama Lg2 nchini Burundi. Kama ilivyodhihirika sasa hapo juu kwenye jedwali Na.5.11 Wajifunzaji hao hutamka lugha ya Kiswahili kwa kuchopeka irabu mbalimbali kama /i/ kwa maneno ya Kiswahili yenye silabi funge, yaani ni kumanisha konsonanti mbili

zifikuatana katika neno moja ndipo tunasema kuwa kunapatikana silabi funge.

Chanzo cha ukakamaaji huo wa uchopekaji kwa wajifunzaji hao Warundi katika mchakato wa ujifunzaji Kiswahili kama Lg2 huwa unajitokeza pale wanafunzi wanafanya ukakamaaji katika kutumia muundo wa silabi wa Konsonanti na Irabu (kuanzia sasa KI) ambao unajulikana kama muundo wa kawaida katika lugha ya Kirundi ambayo ni Lg1 kwao au lugha mama. Jambo hili ndilo aliloshadidia mtalaamu Iribemwangi (2010) aliposema kwamba lugha nyingi hasa za kifarika hupendelea silabi zenye muundo wa KI. Hali hii inakuja kusababisha wanafunzi wanaozungumza Kirundi (Lg1) kutamka Kiswahili ikiwa Lg2 kwa kuchopeka /u/ na /i/ katika maneno ya Kiswahili sanifu kama maneno daktari wanalitamka daktari, neno labda walitamka labuda, neno elfu wakalitamka elufu, neno maktaba wakitamka makataba, n.k. Tukimhusisha mtalaamu na mwanazuoni Massamba (2011) anasema kuwa katika lugha kadhaa (zikiwemo lugha za kibantu) mwambatano wa sauti za aina moja (kama KK au II) haupendelewi sana katika utamkaji wa maneno.

Hivyo, ilidhihirika kwamba kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili ambayo yanaonekana kuwa yana mfuatano wa sauti konsonanti, wajifunzi Warundi wanapotamka Kiswahili kwa njia ya ujifunzaji kama Lg2 huwa wanafanya uchopekaji wa irabu kwa madhumuni ya kuzingatia ule muundo wao wanaouzoea wa KI. Aidha, vokali hizo zinachopekwa ili kuzuia konsonanti zisifuatane. Hali hiyo ndiyo inaonekana inasababisha wajifunzaji hao kufanya ukakamaaji kwenye baadhi ya utamkaji wanaposimulia hadithi darasani. Isitoshe, data ziliigemea wajifunzaji wanaosoma idara za lugha ya Kiswahili ambao wanakuwa na sharia na kaida za lugha husika nyingi zinazoweza kuwasaidia kuzuia huo ukakamaaji. Kadhalika, ni wanafunzi wa mwaka wa tatu digrii vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi ambao hatuwategemei kufanya ukakamaaji kwa kuwa wanakuwa wameanzia kusoma Kiswahili ikiwa Lg2 shule ya msingi hadi vyuo vikuu. Jambo ambalo kwa mujibu wa Bialystok na Miller (1999) wanafafanua zaidi kuwa wajifunzaji wa Lg2 au ya kigeni wanapojifunza takribani miaka mitatu na hatimaye wakaendelea kukakamaa kwa kutamka fonimu mbalimbali, fonimu hizo zinaimarika na kuwa sugu. Ina maana kuwa hao wamekakamaa kama mtalaamu anavyodai hapo juu.

HITIMISHO

Makala hii ilichunguza ukakamaaji wa kimatamshi kwa wajifunzaji wa Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi. Utafiti huu uliongozwa na Nadhariatete Teuzi ya Ukakamaaji ambayo iliasisiwa na Han (2009: 254). Matokeo ya makala hii yamebaini kuwa kunajitokeza fonimu mbalimbali ambazo zilidhihirisha hali ya ukakamaaji kwa wajifunzaji Warundi wakati wanajifunza Kiswahili Lg2. Katika tatizo la utafiti kulibainika uwepo wa shida za matamshi yasiyo sahihi kwa Warundi hasa wale wanaosoma Kiswahili vyuo vikuu vya serikali. Shida hizo ni pamoja na kukakamaa kwa baadhi ya fonimu za Kiswahili wanapojifunza Kiswahili kama Lg2. Tukirejelea katika kazi ya onyango (1997), Ndun'gu (1999), Mutugu (2001) tuliona kuwa watumiaji wengi wa Kiswahili kama Lg2 hukumbwa na matatizo katika matumizi yake ya Lg2. Wazungumzaji wa lugha mbalimbali za asili Kirundi kikiwamo ambao huzungumza lugha ya Kiswahili kama Lg2 nao huathiriwa na sauti za lugha yao katika vipengele mbalimbali vya kiisimu fonolojia ikiwamo. Kama ambavyo mtafiti alivyokuwa bayana katika sehemu ya tatizo la utafiti kuwa kwa ufahamu wake, nchini Burundi Kiswahili kama Lg2 ilikuwa hajafanyiwa utafiti wa kina kuhusiana na suala la ukakamaaji hasa kipengele cha kifonolojia ambacho ametatitia. Hivyo, utafiti huu ulitoa mchango mkubwa kwa watafiti wengine kuhusiana na kuathiriana kwa lugha hasa hizi za Kibantu tukianza Kiswahili na nyingine.

Kadhalika, utafiti huu umekusanya maoni, mitazamo kutoka watoa taarifa mbalimbali ya watumiaji wa Kiswahili kama Lg2 nchini Burundi na kuona namna ya kuweza kuepukana na suala la ukakamaaji.

Matokeo ya makala hii husika ilibaini kuwa kuna aina nyingi za fonimu zilizodhihirisha ukakamaaji kwa wajifunzaji wa Kiswahili kama Lg2 katika vyuo vikuu vya serikali nchini Burundi. Baadhi ya mifano ya aina za fonimu ni kama: ukakamaaji wa /ŋg/ badala ya /ŋ/, ukakamaaji wa sauti /s/ badala ya /θ/, ukakamaaji wa kuchopeka kiyeyusho /w/ mahala kisipotakiwa, ukakamaaji wa sauti /ð/kuwa/θ/, ukakamaaji wa kudondosha sauti /h/ mwanzoni mwa neno, ukakamaaji wa sauti /s/ kutamkwa kama /tʃ/, ukakamaaji wa sauti /d/ badala ya /ð/, ukakamaaji wa sauti /gh/ kuwa /g/, ukakamaaji wa kuchopeka /h/, ukakamaaji wa kuchopeka sauti /u/ na /i/ katika silabi funge silabi. Jambo kama hili linaweka bayana kuwa katika taaluma ya fonolojia, kuliongezwa mchango mkubwa wa kitaaluma hasa kwa watafiti katika uwanja huu wa kimatamshi lakini pia kwa wasomaji vitabu, waandaji mitaala katika kunufaika mengi yanayohusiana na fonolojia na vipengele vyake kwa ujumla. Kwa ufupi tunaweza kusema kabla ya utafiti huu kuna taarifa ambazo zilikuwa bado hazijawekwa wazi. Yaani mwongozo huu ulikuwa haujabainishwa katika uwanja wa fonolojia. Hivyo, utafiti huu utachangia katika tafiti nyingine za baadaye.

MAREJELEO

- Bialystok, E. na Miller, B. (1999) "The Problems of Age in Second Language Acquisition: Influences from language, structure, and task". *Bilingualism: Language Cognition*, juz. 2/2: 127-145.
- Brown, H. D (1994), *Principles of Language Learning and Teaching* (Toleo la 3),
- Brown, H. D (2002), *Principles of Language Learning and Teaching*, (Toleo la nne),
- Chen, C. A. (2009). First language influence and fossilization in second language vocabulary acquisition. *Teachers College, Columbia University Working Papers in TESOL & Applied Linguistics*, 9(2), 65-67.
- Ellis, R. (1985) *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford, Oxford University Field methods. Cambridge: Cambridge University Press.
- Flege J.E. (1995). Second language speech learning: Theory, findings, and problems. In W. Strange (ed.), *Speech perception and linguistic experience: Issues in cross-*
- Flege, J. E. (1992). Speech learning in a second language. In C. A. Ferguson, L. Menn & C. Stoel-Gammaon (Eds.), *Phonological Development Models, Research, Publications*: York Press.
- Gawasike, A. (2016). Ukakamaaji kwa Wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika Jamii ya Wakinga (Haijachapishwa). Tasnifu ya Uzamivu: Kikuu Cha Dar es salaam.
- Guthrie, M. (1948). *The Classification of Bantu Languages*. Oxford: Oxford University Press.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2007). *Msingi wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Han, Z-H. (2009) *Fossilization in adult Second Language Acquisition*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Han, Z-H. (2009) *Interlanguage and Fossilization: Towards and Analytical Modal* Katika Cook, V. na L. Wei (Wah) *Contemporary Applied Linguistics Language teaching and learning*. Juzuu Na.1 (Uk.137- 162). London: Continuum.
- Iribemwangi, P. (2010). *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound changes and Words*. Saarbrücken: Verlag
- Krasen, S. D. (1982) *Principles and Practices in Second Language Acquisition*. Oxford: Pergman. language research. Baltimore: York Press, 2008. p. 233-277. *Learning*, 28, 29-54.
- Long, M. (1997) "Fossilization: Rigor Mortis in Living Linguistics Systems"?
- Long, M. (2003) "Stabilization and Fossilization in Interlanguage Development". Katika Douhy, C. na M. Long (Wah.) *Handbook of second Language Acquisition*. (kur. 487-536), Oxford: Blackwell.
- Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2008), *NADHARIA YA LUGHA.KISWAHILI* 1.Kidato cha 5 Na 6. Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es salaam.
- Massamba, D. P. B. na wenzie. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. TUKI, Chuo
- Massamba, D.P.B. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msanjila, Y. P. na wenzake (2011), *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mtesigwa, C. K. P. (2009) "Utayarishaji wa Vitabu vya Kufundishia Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Haja ya Kuzingatia Mkabala wa Mawasiliano". *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 72: 52-67.
- Mutugu, B.N (2001). *Makosa ya Kileksia na Chanzo Chake*. Uchunguzi washule za Upili Wilayani Kiambu (unpublished master's thesis) Kenyatta University. Nairobi.
- Ndung'u, N. (1999). Monetary and exchange rate policy in Kenya. (AERC Research Paper No 94). Nairobi Kenya: African Economic Research Consortium. New York, Longman
- Ouma-Onyango, R. A. (1997). *Information Resources and Technology Transfer Management in Developing Countries*. London: Routledge.
- Perdue, C. ed. (1993). *Adult language acquisition: Cross-linguistic perspectives*. Volume 1,
- Perdue, C. ed. (1993). *Adult language acquisition: Cross-linguistic perspectives*. Volume 2. The results. Cambridge: Cambridge University Press. Prentice Hall Press. England: Multilingual Matters.
- Preston, Dennis R. (1989). *Perceptual Dialectology*. Dordrecht: foris.
- Schumann, J. H. (1978a). The acculturation model for second language acquisition. In R. C. Gingras (Ed.), *Second language acquisition and foreign language learning*. Washington, DC: Center for Applied Linguistics.
- Schumann, J. H. (1978b). The pidginization process: A model for second language acquisition. Rowley, MA: Newbury House. (209-230)
- Selinker, L. (1972). 'Interlanguage.' *International Review of Applied Linguistics*, (10): 209-230.
- Stauble, A. E. (1978). Decreolization: A model for second language development. *Language*
- Stauble, A. E. (1978). Decreolization: A model for second language development. *Language Learning*, 28, 29-54.
- Stauble, A. E. (1978). Decreolization: A model for second language development. *Language*
- Stern, H. H (1983), *Fundamental Concepts of Language Teaching*, Oxford, Oxford University Press
- Zheng, Y. (2010) *On Some New Models of Instruction for Overcoming Fossilization in English Learning*. North Institute of Science and Technology: China.
